

RUDI
KWA MUNGU

MWANDISHI: ELEZOHAKI

Everyday Publications Inc.
310 Killaly St W
Port Colborne ON L3K 6A6
Canada

ISBN 978-0-88873-185-2

Imprimé au Canada

copyright © 1967 William MacDonald All Rights Reserved

NINI ILIPATA KAHINDO?

Kahindo alikuwa mtumwa wa malofu wakati asipoamini Kristo bado. Alikuwa fundi la matukano vilevile. Kama ungalimwambia ya kwamba siku nyingine atageuka mtu wa Mungu, angalikucheka kabisa. Labda angalikutukana vilevile. Alikuwa askari na alipenda sana kujivuna mbele ya askari wenzake juu ya kipimo cha malofu alichowenza kuywa bila kupata matata . . .

Lakini kulikuwa na askari mmoja katikati yao asiyehehimu Kahindo juu ya mwenendo wake mwovu. Alikuwa Paluku. Paluku aliongoza askari wachache waliokutana kila juma kujifunza Biblia. Yeye na Kahindo walianza kazi ya askari pamoja. Paluku alisemezana naye tena na tena na kumwonyeshea hatari ya njia aliyoofuata na ya kwamba alihitaji Kristo. Kwanza Kahindo alimjibu na ukali, lakin nyuma alifunga masikio yake kwa maonyo ya Paluku. Lakini Paluku alikuwa na saburi — na alidumu kuombea na kuonya Kahindo.

Kahindo alikataa kabisa kukutana na Paluku na rafiki zake kwa kusoma Biblia, lakini mara moja moja aliuliza Paluku maneno yaliyoonyesha njaa ya roho yake.

Usiku mmoja Kahindo alikuwa akirudia camp militaire nyuma ya kunywa malovu na watu wenigne mjini. Njiani watu watatu walimtupa chini, wakampiga, wakaiba mali yake na kumwacha njiani

kama mfu. Watu wengine walimkuta pale nyuma kidogo, wakambeba kwa hopital ya camp militaire, akashinda siku mbili hopitalini.

Majuma mawili nyuma ya maneno haya Paluku alisimama karibu na Kahindo saa walipongoja ku-pewa mshahara wao. Nyuma ya kupokea mali yao walikwenda kutembea kidogo shambani. Paluku alitaka kusemezana na Kahindo juu ya kuamini Kristo na mara hii Kahindo alikuwa tayari kusikiliza. Paluku alimwelezea Habari Njema tena waziwazi, kisha alimwonya kujitoa mzima kwa Bwana.

Na roho ya kuvunjika Kahindo alipiga magoti pale shambani, akaomba, "Mungu, kufika sasa nilikuwa katika giza kubwa, lakini sasa ninaona nuru."

Maisha ya Kahindo yaligeuka kabisa. Hakuwa na kiburi tena na aliachana na desturi zake nyingine za zambi mara moja. Alianza kufikia makusanyiko ya kujifunza Biblia. Pale alijifunza ya kwamba ni sharti kwake kuweka saa kila siku kusoma Biblia peke yake pamoja na kuomba. Alianza kujifunza mashairi ya Biblia kwa nia na alishuhudia Kristo mbele ya askari wenzake.

Kwanza ilikuwa nguvu kwa yeye kuvumilia mazarau ya watu, zaidi wakati alipokuwa katikati ya watu wengi. Saa yenye we alinyamaza kimya, lakini alisemezana na watu mmoja mmoja juu ya Kristo wakati alipopata njia.

Nyuma ya majuma machache askari wenzake waliacha kumzarau na walianza kumheshimu kwa sababu ya mwenendo wake mzuri na kwa namna

alivyoshuhudia Kristo na roho ya mapendo na uhdari.

Kahindo alizidi kupata nguvu katika imani. Ali-komboa Paluku kwa kazi ya kuongoza kusanyiko la kujifunza Biblia wakati Paluku alipotumwa pahali pengine. Watu 35 walipokea Kristo kwa sababu ya mafundisho ya Kahindo.

* * * * *

Miaka sita na zaidi imepita tangu wakati ule. Sasa Kahindo si askari tena lakini amerudi kwa mji wake. Ameoa mke na ana watoto wawili, mtoto mume na msichana. Anafanya kazi ya karani. Lakini hawaki tena kwa Bwana kama mbele. Yeye na mke wake hawafikii hata makusanyiko ya kanisa. Watoto wake hawajafikia école du dimanche bado. Rafiki za Kahindo si Wakristo. Ni kama anajaribu kuepuka kuonana na Wakristo.

Paluku ameacha kazi ya askari vilevile na siku moja alifika kuona Kahindo kwa sababu alikuwa amesikia ya kwamba Kahindo hatembe tena pamoja na Bwana. Walisalimiana na adabu yote, lakini si na urafiki mtamu kama mbele. Upatano wa karibu ambao walikuwa nao mbele ulikuwa ume-potea.

Nyuma ya kuzungumuza kwa dakika chache Paluku aliuliza, "Nini ilitokea, Kahindo? Nini iliku-ondosha karibu na Bwana?"

Kahido hakujibu neno. Alitupa tu cigarette yake chini na kuikanyaga kwa kiatu chake. Paluku ali-jaribu tena, "Kahindo, hakuna mtu anayeweza kuni-

aminisha ya kwamba hukuokolewa kweli siku ile shambani.”

Kahindo aliangalia kwa upande wa nyumba kuona kama watu wengine walikuwa wakisikiliza. Kisha alijibu, “Ndiyo, niliokolewa kweli siku ile . . . lakini sasa mimi ni mbali na Bwana.” Alitazama chini saa aliposema maneno haya na sauti yake ilionyesha huzuni ya roho yake.

Aliokolewa, lakini alikuwa mbali na Bwana! Huzuni kubwa.

Nini ilikuwa imetokea?

Nini iliondosha Kahindo karibu na Bwana?

Ataweza kurudi karibu na Bwana tena?

Namna gani?

NI NYEPESI SANA KWA UPATANO WA MKRISTO NA BWANA KUHARIBIKA

Neno lilitotokea katika maisha ya Kahindo linatoka katika maisha ya Wakristo wengi, ndilo kuru-di nyuma. Mkristo anarudi nyuma na kuacha njia ya Bwana kwa sababu alifanya zambi na alikataa kukiri zambi hii. Mkristo huyu hana upatano mzuri na Mungu tena.

Upatano wa Mkristo na Bwana unaweza ku-haribika namna gani?

Mungu ni mtakatifu naye hana zambi. Hakuna giza ndani yake hata kidogo (1 Yoane 1:5). Mtu akitaka kuwa na upatano mzuri na Mungu inampasa

kukiri zambi zake na kuziacha. Maana ya upatano ni kushiriki pamoja. Namna gani basi watu wawili wanaweza kushiriki ndani ya kazi moja kama wasipokuwa na roho moja na kufikili sawasawa juu ya maneno? Haiwezekani kwa mtu kuwa na upatano mzuri na Mungu kama akikaa kufanya maneno ambayo Mungu alimkataza kufanya (1 Yoane 1:6-7).

Watu wa jamaa moja wana upatano mzuri kama wakikaa na salama na furaha pamoja. Lakini mara nyingine mume na mke wanagombana. Halafu upatano wao unaharibika. Salama na furaha zinakimbia kufika wakati mume na mke wanapokiriana zambi zao na kupatana tena.

Ni vivyo hivyo ndani ya jamaa ya Mungu. Zambi inaharibu upatano wetu na Mungu. Basi namna gani tunaweza kutengeneza neno hili tena? Kuna njia moja tu. Sharti tukiri zambi yetu na kuiacha.

Tumeona ya kwamba saa Mkristo anapofanya zambi, upatano wake na Mungu unaharibika. Basi Mungu anamwondosha ndani ya jamaa yake vile-vile? Sivyo. Wakati mtu anapookolewa anazaliwa tena na anageuka mtoto wa Mungu kwa njia ya imani ndani ya Bwana Yesu Kristo (Yoane 1:12). Neno hili haliwezi kubadilika kamwe.

Nyuma ya kufanya zambi Mkristo ni mtoto wa Mungu kama mbele lakini upatano wake mtamu na Baba yake umeharibika. Angali na uzima wa milele, lakini hana furaha tena rohoni juu ya wokovu wake.

Neno hili linaweza kutokea ndani ya maisha ya kila mwamini. Mara nyingi linaanza wakati mwamini anapopunguza saa aliywewka mbele kwa kusoma Biblia na kwa maombi. Kazi ni nyingi na ni ngu-

vu kwa yeye kupata saa kukaa kimya mbele ya Bwana. Halafu wakati tusiposoma Biblia kila siku hatuhukumu zambi zetu na ukali kama mbele. Hatuchukii majaribu namna tulivyoyachukia mbele na mawazo juu ya zambi yanageuka matamu kwe-tu. Kwanza tunasoma hatuwezi kufanya zambi hizi sisi wenyewe, lakini tunakaa kuwaza juu yao, na nyuma kidogo tunapima nusu nusu, kama kuonja tu, na mwishoni tunazama ndani yao (Yakobo 1:14-15).

Wakristo wengi wanarudi nyuma mara nyininge. Biblia inatupasha juu ya watu wa Mungu wa zamani walioacha zambi kuharibu upatano wao na Mungu: kama Loti, Samusoni, Naomi, Daudi, Yona, Petro, na Dema. Mkristo yule anayefikili hatarudi nyuma kamwe ni katika hatari kubwa zaidi (1 Wakorinto 10:12).

Wakati upatano wetu na Bwana unapoharibika, mara moja Roho Mtakatifu anaanza kutumika ndani yetu kuturudisha karibu na Mungu tena. Anajaribu kutufahamisha ubaya wa zambi zetu hata tuweze kutubu na kuzikiri. Mara nyininge majuma na miezi, hata miaka inapita bule kwa sababu ya kiburi na ugumu wa mioyo yetu.

Ni sharti kwetu kukiri zambi zote mbele ya Mungu. Kama zambi zetu ziliumiza watu wengine, sharti tuzikiri mbele yao vilevile (Matayo 5:23-24), na kulipa vilevile kama walipata hasara kwa sababu yetu.

Basi Mkristo akikwisha kukiri zambi zake na roho ya kweli mbele ya Mungu na kutengeneza maneno yake na watu ambaeo aliwakosea, ana upatano mtamu na Mungu tena.

Ni kusema Mkristo anaweza kufanya zambi bila kupata matata? SIVYO! Tuwaze kwanza juu ya maneno mawili: **Azabu na matunda** ya zambi.

Biblia inafundisha wazi ya kwamba mwamini anayerudi nyuma hataazibiwa na azabu ya milele kama wasioamini. Mwokozi wetu alibeba azabu hii wakati alipokuwa juu ya msalaba. Wale amba wanamwamini hawatafika kwa hukumu lakini wamepita kutoka mauti kuingia uzima (Yoane 5:24). Au kusema, hata mwamini wa kweli akifanya zambi, hataazibiwa katika ziwa la moto. Kristo alili-pa kwa zambi zetu wakati alipomwanga damu yake msalabani na Mungu alikubali zabihu yake. Hataki malipo mara mbili, toka Kristo, na tena kwetu!

Mtoto wa Mungu akifanya zambi, Shetani ana-mshitaki mbele ya kiti cha kifalme cha Mungu. Lakini Bwana Yesu anasimama pale vilevile kama Mwombezi wetu, anaonyesha vidonda mikononi na miguuni mwake na kusema, "Mimi nimelipa kwa zambi ile miaka 1900 mbele!" (1 Yoane 2:1).

Hivi Mkristo anayeacha njia ya Bwana hataazibiwa katika ziwa la moto kwa zambi zake lakini hata hivi itampasa kuvuna matunda machungu ya zambi zake, hapa duniani na mbinguni vilevile.

***Mengine ya matunda ya zambi atakayovuna
kwa wakati wa sasa ndiyo haya:***

1. Jina la Bwana Yesu linazarauliwa.
2. Ushuhuda wake kwa Kristo unaharibika.
3. Watu wengine wanapata huzuni na taabu kwa sababu ya zambi zake.
4. Mali nyingi inapotea bule.

5. Labda atapata ugonjwa wa wili, na hata mafikili yake yatakuwa ovyo.
6. Anapata haya na huzuni nyingi.
7. Kazi Bwana aliyotaka aifanye inachelewa.
8. Watu wengine wanakwaa kwa sababu ya zambi zake.

Matunda ya zambi zake mbinguni:

1. Hatapokea zawabu wakati atakaposimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo (1 Wakorinto 3:15).
2. Hatakaa na furaha nyingi pamoja na Bwana katika utukufu wa mbingu kama mtu yule aliyeetmbea karibu na Bwana duniani.

Lakini hata hivi Mungu ni mkubwa kupita zambi zetu. Anataka mtomboki kurudi kwake. Mlango ni wazi siku zote. Baba atamkaribisha tena na furaha nyingi. Na Bwana anaweza kufanya ajabu kutupatia baraka na kutukuza jina lake hata kama tulifanya zambi.

Tumeona ya kwamba mtu anarudi nyuma wakati anapofanya zambi. Ni zambi inayoharibu upatano wake na Mungu. Upatano huu unaweza kutengenea tena kwa njia moja tu: sharti akiri zambi zake na kuziacha.

WATU WANAONDOKA KARIBU NA BWANA KWA NJIA MBALIMBALI

Wengine wanarudi nyuma kwa sababu ya kutenda zambi ya mwili: Citoyen Bumani alifanya hivi. Alikuwa amekaa pamoja na mke wake kwa

miaka 15 na alishiriki ndani ya kazi ya Mungu kanisani vilevile. Alikuwa tu namna ya Wakristo wote, lakini alifurahia wanawake zaidi. Alipenda kuwaambia maneno matamu na kugusagusa miili yao. Halafu siku moja ilimpasa kufanya safari kwa ajili ya bwana wake wa kazi na kule katika mji mwengine alianguka. Tangu siku ile anafikia nyumba ya Mungu siku moja moja tu. Hana furaha tena nyumbani mwake kama mbele. Watu hawajui nini imetokea na kwa sababu gani roho yake ni baridi naye hakai na furaha pamoja na watu. Anakusudi kuficha zambi yake, lakini hana salama rohoni.

Watu wengine wanafanana na mwana mpote-vu katika Luka 15. Tuwaze juu ya citoyen Bulabanga. Alipata nguvu nyumbani mwa Wakristo na aliokolewa mwaka mmoja mbele ya kuingia kazi ya askari. Alifurahi sana siku alipoondokea nyumba ya wazazi wake na hakuwa chini ya amri yao tena. Alikusudi kutimiza mapenzi yake yote. Askari wenzake hawakuweza kujua ya kwamba yeche ni Mkristo. Alishiriki ndani ya zambi zao zote . . . lakini kule ndani zamiri yake ilimshitaki naye hakuwa na furaha hata kidogo.

Wakristo wengine ni kama citoyen Kularaba aliyeacha njia ya Bwana kwa sababu ya kujifunza zaidi. Mtu huyu alikuwa mwenye akili nyingi. Nyuma ya kumaliza chuo ya Biblia alikwenda kwa chuo cha elimu nyingi. Alitaka sana kuendelea na alijifunza elimu ya asili ya mambo yote na vitu vyote. Nyuma ya mwezi mmoja tu alipata shaka rohoni juu ya imani yake kwa sababu ya mafundisho aliyopata pale. Hakuwaka tena kwa

Bwana. Aligeuka mtu wa kasirani na roho yake ili-jazwa mashaka na maulizo.

Wakristo wengine wanageuka walevi, kama citoyen Namutali. Alianza kunywa malofu nusu nusu tu wakati alipokuwa nyumbani mwa watu wengine, lakini alikunywa zaidi saa alipokuwa na masumbuko nyumbani au wakati kazi ilipoongeze-ka kupita kipimo. Sasa pombe inamtawala kabisa. Anapata haya kubwa kila mara anapowaza juu ya kanisa na rafiki zake Wakristo. Halafu anakunywa chupa kingine cha pombe kwa kulalisha zamiri yake.

Wakristo wengine wanarudi nyuma kwa sababu wameoa mskiyeamini. Tubakori alikuwa msichana wa furaha aliyependa Bwana sana. Alipasha rafiki zake zote habari za Mwokozi wake. Kijana mmoja alipatana naye kwa kumwoa na nyuma ya majuma machache kijana huyu alisema kwamba ameamini Kristo vilevile. Leo Tubakori anafikili mume wake hakuamini kweli kweli. Yeye na mume wake hawa-shiriki pamoja ndani ya maneno ya Mungu na nyumba yao ni nyumba ya magomvi tu. Watoto wao hawaijui kutii. Mume wake anamwambia Tubakori ya kwamba hampendi na hapendi watoto wake. Kila mangaribi nyuma ya kazi anakwenda kukaa pamoja na rafiki zake, akiacha Tubakori peke yake nyumbani na huzuni na machozi. Tubakori alijaribu kufuata Bwana kwa miaka michache nyuma ya kuolewa, lakini sasa ameacha.

Wakristo wengine wanarudi nyuma kwa sababu ya kazi yao. Hawafanyi zambi kubwa sana lakini wanaacha kazi yao kula saa zao zote hata hawana saa tena kwa jamaa yao wala kwa Mungu. Ha-

waweki saa kwa kusoma Biblia na kwa maombi na wanakutana pamoja na Wakristo wengine kuabudu Mungu siku moja moja tu. Masumbuko ya maisha ya sasa yamepunguza nguvu yao ya roho na kuwa-acha zaifu sana kwa maneno ya Mungu. Tamaa na mapendo ya mali yamewashinda.

Wakristo wanarudi nyuma kwa njia mbalimbali kabisa. Wengine wanapata hasara na halafu roho zao zinageuka baridi. Hawakubali ya kwamba mambo haya ni mapenzi ya Mungu kwa maisha yao. Hawafahamu ya kwamba taabu yao itageuka baraka kwao nyuma, hivi wanakasirika na kupoa rohoni.

Wengine wanakataa kusamehe watu wengine ambao waliwaumiza. Wanakaa na roho nguvu, bila rehema. Basi Mungu Baba hawezi kusamehe wato-to wake wanaokataa kusamehe ndugu zao (Matayo 6:14-15).

Wakristo wengi wanarudi nyuma kwa sababu ya magomvi madogo madogo nyumbani mwao. Mume na mke hawakai tena na salama na mapendo pa-moja. Inawashinda kusemezana vizuri, na haw-ombi tena pamoja. Wao wawili wanakataa kukubali ya kwamba wameanguka. Roho zao ni ngumu ka-ma chuma na hawafahamu ya kwamba wao wawili walikuwa wamekwenda mbali na Bwana.

Kwa nini watu wanarudi nyuma? Kwa sababu ya zambi. Wanaasi maagizo ya Mungu, wanaacha tamaa ya mwili kuwatawala, wanapenda mali na vitu vya dunia hii kupita Mungu, wanakataa ku-samehe wenzao, vivi hivi.

Unashangaa kusikia ya kwamba waamini wana-weza kwenda mbali na Mungu hivi? Tukumbuke

kwamba watu wa Mungu wa zamani walirudi nyuma vilevile:

- 1) Daudi alirudi nyuma kwa sababu ya tamaa ya mwili. Alizini na kuua mtu (2 Samweli 11:1-27).
- 2) Mungu aliokoa Noa toka garika, lakini nyuma yake Noa alishindwa na ulevi (Mwanzo 9:20-21).
- 3) Loti alirudi nyuma kwa sababu ya kazi yake. Alitafuta heshima na utajiri katika mji wa Sodomo (Mwanzo 13:7-11; 19:1-28).

Watu hawa wote walitubu na kurudi karibu na Mungu. Walikuwa na upatano mzuri naye tena. Basi kila mwamini wa kweli aliyeacha njia ya Bwana anaweza kurudi karibu naye vivyo hivyo kama akitubu na kuacha zambi zake.

KATIKA INCHI YA MBALI

Moja ya alama za kwanza zinazoonyesha ya kwamba Mkristo anapoa rohoni ni mavumbi juu ya Biblia yake. Haweki roho tena juu ya kusoma Neno la Mungu kila siku. Bado kidogo siku chache zinapita naye hajafungua Biblia yake bado, nyuma yake juma zima linapita bule, na mwishoni anaacha kabisa kusoma Neno la Mungu. Maandiko Matakatifu si matamu tena kwake.

Ni vivyo hivyo na maombi yake. Mbele aliweka roho sana juu ya maombi. Alifahamu ya kwamba ilimpasa kushinda kwa maombi ili maisha yake yawefe kuwa na faida kwa Bwana. Lakini sasa anaomba mara moja moja tu na ni kama maombi haya ni bule, hayana uwezo na hayafikii masikio ya Mungu.

Hafikii tena makusanyiko yote ya kanisa kama mbele. Mafundisho anayosikia pale yanachokesha

roho yake. Anawaza watu wengi kanisani ni wadanganyifu tu. Vizuri aache kwenda kanisani basi . . . Halafu Wakristo wanaanza kusumbuka juu yake na kujaribu kumrudisha tena karibu na Bwana, lakini akili yake inashinda akili yao naye anawaepuka kila mara. Ni machukizo kwake sasa kukaa pamoja na waamini.

Hesabu ya rafiki zake **wasio** Wakristo inaongezeka saa zote na anashiriki nao ndani ya maneno yao. Kwa mwanzo zamiri yake ilimchokoza kidogo juu ya kushiriki ndani ya maneno ambayo mama yake aliiita “maneno ya dunia”, lakini nyuma kidogo hasikii sauti hii ndogo tena rohoni mwake na anashiriki na salama na adabu yote na wasioamini wale.

Lakini tena na tena maneno yanatokea kumkumbusha ya kwamba ye ye ni katika hatari kubwa. Bila kufahamu watu wanasema maneno yanayotoba roho yake. Anasoma au kusikia maneno yanayochokoza zamiri yake ndani ya barua, radio, vitabu, lakini anaona yote bule.

Hafurahii wokovu wake tena. Mbele aliweza kuwaambia watu habari za Yesu na akili na furaha, lakini sasa neno hili haliwezekani tena. Mbele aliimba nyimbo za wokovu na ushuhuda na furaha nyingi. Anaimba sasa vilevile, lakini anatumia kitabu cha muziki ya dunia, si nyimbo za Bwana.

Amefungwa na desturi ya kunungunika juu ya maneno yote. Labda ni hivi kwa sababu maneno yake yanazidi kukologana sasa. Ni kama ana bahati mbaya siku zote. Halafu anataabisha watu wengine kwa sababu maneno yake mwenyewe

hayatembei vizuri. Zamani alisemezana na watu na roho nzuri na adabu, lakini sasa masemo yake ni makali siku zote.

Ilikuwa nguvu kwa yeye kufanya zambi fulani mara ya kwanza, lakini mara ya pili ilikuwa nyepesi. Basi anazidi kuendelea ndani ya zambi.

Halafu anajaribu kuhakikisha mwenendo wake wa sasa na anapata mashairi ndani ya Biblia kumsimamia ndani yao. Anafikili kuna watu wengi wanaoonekana kama Wakristo wazuri, lakini wanaoanya zambi kubwa kupita zambi yeye anazotenda. Nyuma kidogo anajidanganya kabisa kwa njia ya kufikili kwamba zambi fulani si zambi kweli kama akizitenda na mapendo.

Anakaa na uchungu tu rohoni. Akikwama ndani ya zambi, hawezi kuwa na furaha kwa sababu anajua Neno la Mungu linamkataza kuzitenda. Lakini hawezi kukubali ya kuwa ana huzuni. Anajua namna gani kudanganya watu na kuwaaminisha kwamba anakaa na furaha tu. Hataki hata kidogo kukiri mbele ya watu taabu na uchungu zinazojaza moyo wake.

Anajaribu siku zote kuficha mwenendo wake mwovu na anakaa na woga ya kwamba siku nyiningine atapatikana. Labda analipa watu wengine mali, kuwanyamazisha, wasiwaambie watu wengine habari zake.

Mara nyiningine yeye mwenyewe anashangaa juu ya matata anayopatikana nayo. Anafahamu kwamba hata rafiki zake Wakristo walio masikini zaidi wanakaa vizuri kupita yeye. Ni kama ameingia mtego na hawezi kujiondosha ndani yake.

Masemo yake yamegeuka kabisa na hata rafiki

zake wasioamini wanamhamakia juu ya kinywa chake kichafu. Haya kabisa kukemewa hivi na wapagano!

Kuna neno lingine ambalo linaumiza roho yake. Ni ushuhuda wake kwa Kristo. Anaona ya kwamba wengi wa rafiki zake wanahitaji Kristo kabisa, lakini anaweza kuwaambia nini? Wengine wanamwuliza maneno na kumpa njia kushuhudia Bwana. Lakini ni kama midomo yake imefungwa na ufunguo. Siku moja alijaribu kusaidia mtu mmoja na maneno ya Mungu, lakini mtu huyu alisema naye, "Kama ukiamini maneno haya, wewe ni kwa pahali hapa kwa sababu gani?" Nyuma yake alifikili vizuri anyamaze basi.

Siku moja alifanya zambi mbaya sana namna msiyeamini mmoja mmoja tu anayoweza kufanya. Hata sasa anashituka kabisa rohoni wakati anapofikili juu ya siku ile. Angependa kusemezana na mtu mwingine juu ya neno hili, lakini nani ataweba kufahamu mawazo yake? Hivi anafunga taabu yake yote ndani ya roho yake.

Anashangaa vilevile kuona ya kwamba mapeendo yanaweza kugeuka machukio. Mbele alipenda mtu yule aliyeshiriki pamoja naye ndani ya zambi zake, lakini sasa anamchukia kabisa (2 Samweli 13:15).

Anatumika kazi nyingi, lakini hapati mali. Ni kama mali zinavuya toka mikono na mifuko yake kama maji. Motokari yake ilitwangana na ile ya mtu mwingine na ilimpasa kulipa mali nyingi kwa kuiteengeneza tena. Na siku moja moto ulianza kuteketeza nyumba yake. Hata leo hafahamu kama moto huyu ulianza namna gani.

Alikuwa na deni kubwa karibu na mganga vile-

vile. Alifikia mganga tena na tena, lakini ilishinda mganga kufahamu ugonjwa gani ilimtesa. Hivi alibaki na kuuma kama mbele.

Anakaa kutaraji ya kwamba nyuma kidogo maneno yake yatageuka na kuwa mazuri tena. Maisha yake hayawezi kuwa mabaya hivi daima! Labda kama citoyen Bumani angekufa, maneno yake mwenyewe yangetengenea. Hivi anakaa kungojea mauti ya Bumani, lakini Bumani anakaa na afya njema tu. Basi akifa ye ye mwenyewe, labda maneno yake yangeweza kutengenea? Ndiyo, anawaza hata juu ya kujiuwa mwenyewe . . .

MWISHO WA TUMAINI

Mtu akiwa Mkristo wa kweli hawezi kukaa mbali na Bwana daima. Baba Mungu atapiga mtoto wake kwa kumrudisha tena karibu naye.

Labda itakuwa kwa njia ya kumwondolea mtoto ambaye anampenda sana.

Labda Mungu atamwacha kupata ugonjwa wa nguvu na pale hopitalini wakati anapolala juu ya kitanda chake majuma na miezi anapata saa nzuri kuwaza juu ya zambi zake.

Labda Mungu atampiga kwa njia nyingine . . .

Mbele alijaribu kutoa uzuru kwa mwenendo wake mwovu, lakini sasa anachoka na maneno haya yote na anafahamu hawezi kujisaidia mwenyewe. Saa ile ile anasikia sauti ndogo ndani ya roho yake inayosema:

“Umezama kabisa. Si faida kwa wewe kujaribu kuacha zambi zako. Hata ukiacha zambi zako, utaweza kweli kuishi na furaha tena pamoja na

ndugu zako Wakristo kama mbele? Haitawezekana hata kidogo. Hutaweba kamwe kuacha njia una-yotembea ndani yake. Hakuna tumaini kwa wewe.”

SAUTI INAYOSEMA: RUDI TENA

Halafu katika giza la roho yake anasikia sauti nyingine, sauti tamu. Sauti hii inasema:

“Unaweza kurudi karibu na Mungu. Yeye ni tayari kukupokea. Mungu anaweza kusamehe zambi zako zote, na kukusafisha ndani ya dakika moja tu. Unaweza kuanza tena kuishi kwa Mungu na inawezezana kwa maneno yako kuwa mazuri tena, hata mazuri kupita mbele, kwani hakuna neno linaloweza kushinda Bwana. Kwa nini basi hurudi tena kwa Bwana?”

SIKU YA KUCHAGUA

Halafu inampasa kuchagua nini atafanya. Kuna vita rohoni mwake. Ni haya kwake kukubali ya kwamba alianguka na kufanya zambi, lakini ana hamu kubwa kurudi karibu na Bwana na kute-ngeneza maneno yake tena.

Wakati anapoanza kufikili juu ya kurudi karibu na Bwana, mara moja sauti nyingi zinapiga kelele ndani ya roho yake kumzuiza asirudi karibu na Bwana. Halafu anasikia sauti ya Mungu tena, sauti ya upole na mapendo. Sauti hii inasema, “Rudi kwa Bwana, Mungu wako; kwa maana umeanguka kwa sababu ya uovu wako” (Hosea 14:1).

Nyuma ya kusikia sauti hii vita ndani ya roho yake inakwisha na anaanza kutoa machozi. Kiburi yake inapotea pia. Na sauti inayotetemeka anaanza kuomba,

“Unirehemu, Ee Mungu, sawasawa na wema wako; sawasawa na wengi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi zangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba.

“Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe; ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu; na uzime maovu yangu yote.

“Umba moyo safi ndani yangu, Ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiniondolee Roho yako Mtakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya tayari.

“Halafu nitafundisha wenyе makosa njia zako; na wenyе zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, Ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu; ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupe-ndezwi na zabihu, au ningeitoa, hufurahi kwa sada-ka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, Ee Mungu” (Zaburi 51:1-17).

“Nimefanya zambi juu ya mbingu na mbele yako, sistahili tena kuitwa mwana wako; unifanye kuwa kama mmoja wa watumishi wako wa mshahara” (Luka 15:18-19).

Ni kama nyuma ya maombi haya mzigo mzito unaondoka kwa roho yake. Anakumbuka masemo ya mtume Yoane, “Tukikiri zambi zetu, yeeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote” (1 Yoane 1:9). Anakwamana na ahadi hii na nguvu.

Halafu anakumbuka kwamba mwana mpotevu alirudi karibu na baba yake na baba yake alimkaribisha vizuri sana.

“Akaondoka, akakwenda kwa baba yake. Alipo-kuwa angali mbali, baba yake akamwona, akamhurumia, akapiga mbio, akamwangukia shingo lake, akambusu sana. Yule mwana akamwambia: Baba, nimefanya zambi juu ya mbingu na mbele yako; sis-tahili tena kuitwa mwana wako. Lakini baba aka-waambia watumwa wake: Leteni hapa vazi lililo bora, mukamvalishe, mumpe pete kwa kidolo chake, na viatu kwa miguu. Na leteni kinda la ngombe mwenye kunona, ukalichinje, tupate kula na kufurahi” (Luka 15:20-23).

Anawaza zaidi juu ya maneno haya, “. . . baba yake . . . akapiga mbio, akamwangukia shingoni, akambusu sana.” Anafahamu ya kwamba Baba Mungu alimtendea yeeye vivyo hivyo na anafurahi sana . . .

KURUDI KATIKATI YA WAKRISTO

Hata furaha ikijaza roho yake sasa, anakaa kusumbuka juu ya neno moja, ndilo kukutana tena na

jamaa yake na rafiki zake Wakristo. Haya inataka kumshinda wakati anapowaza juu ya neno hili. Watampokea namna gani? Anaogopa ya kwamba hawatakuwa na furaha kumwona au ya kwamba watamhamakia.

Anakumbuka habari za Naomi katika Agano la Kale. Wakati Naomi aliporudia Betelehemu nyuma ya kuacha njia ya Bwana na kwendea inchi ya Moabu watu waliuliza, "Huyu ni Naomi?"

Naomi aliwajibu, "Musiniite Naomi, muniite Mara; kwa sababu Mwenyezi amenitendea mambo machungu sana. Nilitoka nikijaa, na Bwana amenirudisha bule" (Ruta 1:19-21).

Mkristo aliyerudi karibu na Bwana anawaza, "Mimi ni kama Naomi. Vizuri watu waniite mchungu. Nilikwenda zangu nikibarikiwa sana, na Bwana amenirudisha bila kitu."

Lakini aliogopa bule. Ndugu na rafiki zake wanamkaribisha vizuri sana. Wanashika mkono wake na furaha nyingi, wanamkumbatia, na wengine wanatoa hata machozi. Hakuna mtu anayesema neno kumshitaki juu ya maneno aliyofanya. Wote wanafurahi kumwona.

Anajaribu kuwapasha ya kwamba anahuzunika sana kwa sababu alihayarisha jina la Bwana na kuhuzunisha watu wa jamaa yake na Wakristo wa kanisa. Wanafunga kinywa chake mbio na kumwambia ya kwamba wamemsamehe. Kisha wanashukuru Bwana kwa sababu alijibu maombi yao na kurudisha rafiki yao katikati yao tena. Mkristo aliyerudi alifikili watamhamakia kabisa, lakini sivyo; wanamwonyeshea rehema na mapendo tu.

Mkristo huyu anafurahi sana sana kuwa na upatano mzuri na Bwana na watu wake tena. Furaha ya wokovu wake inajaza roho yake tena. Anashangaa sana juu ya mzigo mkubwa ulioondokea roho yake. Sasa hashindani na Bwana tena na kukimbia Wakristo. Furaha kubwa inajaza roho yake kwani amerudi karibu na Baba yake, na ndugu zake zote walimpokea vizuri.

KUJUA KABISA KWAMBA UMESAMEHEWA

Ni tamu sana kwa mtomboki kuwa karibu na Bwana tena, lakini hata hivi anabaki na masumbuko mengi. Waamini wengi wanaorudi karibu na Bwana wanapata mashaka rohoni na wanafikili labda Mungu hakuwasamehe kweli.

Tuwaze juu ya maneno mengine ambayo yanawafazaisha. Wengine wanauliza,

1. Namna gani ninaweza kujua ya kwamba Mungu amenisamehe?

Unaweza kujua kwa njia ya Neno la Mungu. Mungu ameahidi tena na tena kuwasamehe wale wanaokiri na kuacha zambi zao. Neno la Mungu haliwezi kubadilika. Ukitaka kujua ya kwamba Mungu amekusamehe inakupasa kuamini Neno lake. Waza juu ya ahadi hizi toka Biblia:

“Yeye anayefunika makosa yake hatasitawi; lakini ye ye ambaye anayakiri na kuyaacha atapata rehema” (Mezali 28:13).

“Nimezima makosa yako kama wingu zito, na zambi zako kama wingu; rudi kwangu, kwa maana nimekukomboa” (Isaya 44:22).

“Mtu mbaya aache njia yake, na mtu asiyé haki aache mafikili yake; na arudi kwa Bwana, naye atamrehemu; na kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa” (Isaya 55:7).

“Kujeni turudi kwa Bwana; kwa maana amepasua naye atatuponyesha; amepiga naye atatufungia kitambaa” (Hosea 6:1).

“Tukikiri zambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote” (1 Yoane 1:9).

2. Ninajua Mungu alinisamehe siku nilipoamini Kristo, lakini tangu siku ile nimefanya zambi mbaya sana. Inanishinda kuamini ya kwamba Mungu anaweza kunisamehe zambi hizi!

Daudi alifanya abara na aliua mtu, lakini Bwana alimsamehe (2 Samweli 12:13).

Petro alikana Bwana mara tatu, lakini Bwana alimsamehe (Yoane 21:15-23).

Mungu hakuahidi kusamehe wasioamini tu. Ameahidi kusamehe vilevile Wakristo waliokwenda mbali naye na halafu wametubu na kurudi tena kwake:

“Nitaponyesha kurudi nyuma kwao, nitawapenda sana. Kwa maana kasirani yangu inageuka mbali naye” (Hosea 14:4).

Mungu alitusamehe wakati tulipokuwa adui zake. Kwa nini basi atakataa kutusamehe sasa wakati sisi ni watoto wake?

“Kama wakati tulipokuwa adui, tulipatanishwa na Mungu kwa kufa kwa Mwana wake; zaidi sana

nyuma ya kupatanishwa, tutaokolewa kwa uzima wake” (Waroma 5:10).

Wale wanaoogopa ya kwamba Mungu hawezi kuwasamehe ni karibu sana na Bwana kwani Mungu atakataa kamwe kusamehe mwenye roho ya kuvunjika (Isaya 57:15). Anashindana na wenye kiburi, lakini hawezi kuzarau mtu yule anayetubu kweli kweli (Zaburi 51:17).

3. Hili ndilo ulizo la wengine: **Mungu atanisamehe mara ngapi? Nimetenda zambi fulani na Mungu alinisamehe. Lakini nyuma yake nilifanya zambi hii tena, na tena. Mungu atakaa kunisamehe?**

Tunapata jibu kwa ulizo hili katika Matayo 18:21-22,

“Kisha Petro akamkwenda akamwambia: Bwana, ndugu yangu anikosee mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia: Sikuambii, Hata mara saba; lakini makumi saba mara saba.”

Hapa Bwana anafundisha ya kwamba inatupasa kusameheana mara 70 mara 7, au kusema mara nydingi, bila hesabu. Basi Mungu akitufundisha sisi kufanya hivi, ye ye mwenyewe atafanya vivyo.

Kujua maneno haya hakutupi sisi ruhusa kufanya zambi. Neema ya kushangaza ya Mungu ingepasa kutusukuma kujaribu sana kuepuka zambi.

4. Wengine wanasema: **Lakini sisikii rohoni mwangu ya kwamba nimesamehewa.**

Si kusudi la Mungu kwa sisi kujua ya kwamba tumesamehewa kwa sababu tunasikia hivi ndani ya roho zetu, kwani labda nyuma ya siku moja au mbili hatutasikia neno hili tena rohoni mwetu.

Mungu anataka **tujue** ya kwamba tumesamehe-wa. Ametupa sisi Kitabu chake kutujulisha neno hili. Neno lake, ndiyo Biblia, haliwezi kubadilika kamwe nalo linasema ya kwamba tukikiri zambi zetu Mungu atazisamehe (1 Yoane 1:9).

Ni neno kubwa sana **kujua** ya kwamba ume-samehewa, hata wakati usiposikia hivi rohoni mwako. Inawezekana kwa mtu kusikia ndani ya roho yake kwamba amesamehewa, naye hakusamehewa hata kidogo. Hivi maneno anayosikia rohoni mwake yanamdanganya. Inawezekana kwa watu kusamehewa kweli, lakini watu hawa hawasikii hivi ndani ya roho zao. Kama Mungu ame-wasamehe kweli kweli, si neno kama wakisikia nini rohoni mwao!

5. Kuna wengine wanaosema: **Ninaogopa ya kwamba nimefanya zambi isiyoweza kusamehewa saa nilipokwenda mbali na Bwana.**

Kurudi nyuma si zambi isiyoweza kusamehewa. Katika Agano Jipyा tunasoma juu ya zambi tatu zisizoweza kusamehewa:

1. Bwana Yesu alifanya maajabu yake kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Halafu mtu akisema ali-yafanya kwa uwezo wa Shetani anafanya zambi isiyoweza kusamehewa. Ni kusema Roho Mtakatifu ni Shetani, hivi ni kutukana Roho Mtakatifu (Matayo 12:22-32).
2. Mtu akisema yeye ni mwamini na nyuma anakan Kristo kabisa anafanya zambi isiyoweza kusamehewa. Tunasoma juu ya zambi hii katika Waebrania 6:4-6. Si kukana Kristo namna Petro alivyofanya kwani Petro alirudi tena karibu na

Bwana. Mtu anafanya zambi hii wakati anapokanya Mwana wa Mungu na kusudi na kuhesabu damu yake kuwa kitu kichafu, na kutukana Roho ya neema (Waebrania 10:29).

3. Mtu anayekufa bila kuamini Kristo amefanya zambi isiyoweza kusamehewa (Yoane 8:24). Hii ndiyo zambi ya kukataa kuamini Bwana Yesu Kristo. Mtu wa namna hii anakufa bila imani na bila kutubu.

Mwamini wa kweli ni namna nyingine na mtu asiyeokolewa. Mwamini anaweza kuanguka tena na tena, na halafu kurudi karibu na Bwana tena.

“Hatua za mtu zinasimamishwa na Bwana naye anafurahi katika njia yake. Akianguka, hatatupwa kabisa; kwa maana Bwana atamtege-meza kwa mkono wake” (Zaburi 37:23-24)

“Mtu mwenye haki anaanguka mara saba naye anasimama tena: lakini waovu wanaangamizwa na mabaya” (Mezali 24:16).

6. **Watu wengine wanaamini ya kwamba Mungu aliwasamehe, lakini hata hivi wanakaa kuhuzuni-ka juu ya zambi zao.**

Karibu Wakristo wote wanafahamu uzaifu wao na wanahuzunika kwa sababu waliacha njia ya Bwana mara nyingine. Lakini kwa nini nitakaa kuhuzunika juu ya zambi zangu wakati Mungu anapokwisha kunisamehe? Kwa imani ninaweza kupokea usamehe wa Mungu na kukumbuka maneno yaliyopita kama maonyo tu nisiende mbali na Mungu tena.

MATUNDA YA KURUDI NYUMA

Labda maneno uliyosoma ndani ya kitabu hiki yanakuleta kufikili ya kwamba mtu anaweza kufanya zambi bila kupata matata. Labda unafikili anahitaji tu kukiri zambi zake na kuziacha, hivi zambi si neno kubwa.

Sivyo! Vizuri tufahamu kwamba usamehe wa zambi ni mbalimbali na matunda ya zambi.

Tumeona mbele ya kwamba kuna namna mbili za usamehe:

1. Wakati mtu anapoamini Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wake, Mungu Mwamuzi anamsamehe zambi zake kwa sababu ya kazi Kristo aliyofanya kwa Kalvari (Yoane 3:18). Mwenye zambi aliyesamehewa hataazibwa kamwe kwa zambi zake kwa sababu Mwokozi aibeba azabu hii juu ya msalaba (2 Wakorinto 5:21).
2. Wakati mwamini aliyefanya zambi anapokiri zambi yake Mungu Baba anamsamehe na kumrudisha kwa upatano mzuri naye ndani ya jamaa ya Mungu (1 Yoane 1:9).

Lakini sharti tukumbuke ya kama zambi zinazaa matunda na mara nyingine matunda haya yantaabisha watu kufika mwisho wa maisha yao na hata kwa milele. Tunaona neno hili tena na tena ndani ya Agano la Kale.

1. Abrahamu alioa Hagari saa alipokuwa mbali na Bwana (Mwanzo 16:1-16). Wazao wa Hagari, ndio Waisimaeli, ni adui wakali wa Waisraeli tangu zamani na hata sasa.

2. Kwa sababu ya kurudi nyuma Loti alipoteza mke wake, waume wa binti zake, ushuhuda wake kwa Mungu, na alikuwa karibu kupoteza hata uzima wake (Mwanzo 19:14-26). Alikuwa baba ya Wamoabu na Waamoni, ndio adui wakali wa Waisraeli (Mwanzo 19:14-26).

3. Samusoni aligeuka mfungwa wakati alipokwenda mbali na Mungu. Hakuwa na ushuhuda kwa Mungu tena, aligeuka kipofu, na mwishoni aliuwawa (Waamuzi 16).

4. Naomi aliondoka kwa njia ya Bwana na alipoteza mume wake na wana wake wawili (Ruta 1:3,5).

5. Mungu alisamehe zambi za Daudi, lakini ilipasa Daudi kulipa mara ine kwa uuaji wa Uria: watoto wake wane walikufa:

- (1) Mtoto ambaye Batiseba alimzaa alikufa (2 Samweli 12:19).
- (2) Amunoni aliuawa na ndugu yake Abusaloma (2 Samweli 13:28-29)!
- (3) Abusaloma aliuawa na Yoabu na watu wake (2 Samweli 18:14-15).
- (4) Adoniya aliuawa na Benaya (1 Wafalme 2:24-25).

Mungu alimwambia Daudi ya kwamba upanga hautaondokea jamaa yake kamwe na ilikuwa hivi tu (2 Samweli 12:10).

Daudi alitaka kujengea Bwana hekalu, lakini Bwana hakumruhusu kufanya hivi kwa sababu ya zambi yake (1 Mambo 22:8).

Tunaona matunda ya zambi za Daudi hata leo. Zambi yake iliwapa adui za Bwana njia ya kumtukana (2 Samweli 12:14). Hata leo wasioamini

wanatukana Mungu kwa sababu aliita Daudi mtu aliyependeza roho yake wakati Daudi alipokwisha kufanya zambi kubwa.

Nani anayeweza kujua kipimo cha uchungu wale wanaorudi nyuma wanaovuna! Miezi na miaka Mkristo aliyoshinda mbali na Bwana inapotea yote bule, na zawabu yake kwa kiti cha hukumu cha Kristo kinampotelea vilevile. Alikwaza watu wenngapi kwa njia ya mwenendo wake mwovu? Tena na tena wazazi wanaona watoto wao wakitenda zambi ambazo wao wenyewe walizifanya. Na watoto wengine wanaacha njia ya Bwana kwa sababu ya zambi za wazazi wao!

Kweli haiwezekani kwa Mkristo kurudi nyuma na kufanya zambi bila kupata taabu na huzuni. Tusi-sahau kamwe ya kwamba “yo yote mtu anayopanda, ndiyo atakayovuna” (Wagalatia 6:7).

KUENDELEA PAMOJA NA BWANA

Wakristo wanaoacha njia ya Bwana wanalipa bei kubwa, lakini asante kwa sababu Mungu wetu ni Mungu anayependa kurudisha watomboki karibu naye. Anataka sana Mkristo aliyerudi kwake kushinda zambi zile ambazo zilimwangusha mbele na kufuata Bwana karibu karibu kwa utukufu wake.

Mkristo atawenza kufanya hivi namna gani? Nini itamzuiza asifanye zambi hizi tena?

1. Neno la kwanza ambalo inampasa kufanya ni kuharibu vitu vyote vilivyokuwa kikwazo kwake mbele. Labda ni vitabu fulani au dawa au sanamu au hata mavazi ambayo yanamkumbusha zambi alizofanya mbele. Yuda anatufundisha kuchukia

hata vazi lililotiwa uchafu na mwili (Yuda 23). Mkristo anayefungana na vitu ambavyo vinaamsha tamaa ya mwili anaonyesha kwamba hakutubu kweli au hafahamu ya kwamba hawezi kushinda majaribu kwa nguvu yake mwenyewe.

2. Akitaka kuwa na upatano wa karibu na Bwana kila siku inampasa kukiri mara moja zambi yo yote anaifanya. Wakati anapofahamu ya kuwa ame-anguka sharti ahukumu zambi hii mara moja mbele ya Bwana (1 Wakorinto 11:31).

3. Sharti ajitoe mzima kwa Bwana kufanya mapenzi yake tu (Waroma 12:1-2). Inampasa kujitoa hivi tena na tena, si mara moja tu. Tukijitoa kufanya mapenzi ya Mungu tunakaa na salama, lakini tukifanya kutaka kwetu wenyewe tunajilingiza ndani ya hatari.

4. Ni sharti kabisa kwa mwamini kusoma Biblia kila siku na kutii maagizo anayoona pale (Zaburi 119:9,11). Neno la Mungu linatuonya tusianguke, linatuonyeshea njia ambayo inatupasa kutembea ndani yake na linatupa sisi nguvu kushinda majaribu. Lakini haitoshi **kusoma** tu Neno la Mungu; sharti **tutii** vilevile maneno yo yote ambayo Bwana anatuagiza (Yakobo 1:22). Sharti tunyenyekee Neno la Mungu kabisa kabisa (Isaya 66:2).

5. Sharti mwamini awe mtu wa maombi (Wafilipi 4:6-7). Kuomba ni kusemeza na Mungu juu ya maneno yote ya maisha yetu, maneno makubwa na madogo, na kukubali ya kwamba yeeye ni Bwana wetu. Sharti tuombe vilevile, “Utuokoe na yule mwovu” (Matayo 6:13).

6. Kukutana na Wakristo wa kanisa kila mara kutasaidia Mkristo vilevile kutembea katika utakati-

fu (Waebrania 10:25), kwani kutampatisha nguvu rohoni (Mezali 27:17). Kukumbuka Bwana kila mara kwa njia ya kuvunja mkate kutamsaidia vilevile asifanye zambi (1 Wakorinto 11:23-34).

7. Vizuri mwamini ajaze saa zake na mikono yake na kazi ya Bwana (Waefeso 5:15-16). Saa tunapokaa bule majoribu yanafika kwetu na uwezo mkubwa. Hivi tukikomboa wakati na kufanya kazi ya Bwana, tunajisaidia wenyewe tusianguke (Mhubiri 9:10).

8. Ni vizuri vilevile kwa mwamini kujifunza kuamini na kutegemea Bwana kwa mahitaji yake yote. Bwana anataka tuishi kwa imani, lakini sharti sisi vilevile tuchague kufanya hivi. Sisi watu hatupendi kuishi namna hii. Tunapenda kujiwekea akiba ya mali na kutegemea mali hii kutuchunga. Maana ya kutembea kwa imani ni kukaa na furaha na salama kama tukiwa na chakula na mavazi tu (1 Timoteo 6:8) na kutumia mali yo yote tuliyo nayo zaidi ya ile kwa kazi ya Bwana, tukiamini ya kwamba yeye atatupa sisi vitu tutakavyohitaji kwa wakati wa kuja.

9. Mwishoni, ni sharti kwa Mkristo asiyetaka kurudi nyuma tena kujitoa kwa Bwana tena na tena na kusemezana na Bwana juu ya maneno yote anayofanya.

“Tumainia Bwana kwa moyo wako wote, wala usitegemee ufahamu wako mwenyewe; katika njia zako zote umkiri yeye, naye ataongoza mapito yako” (Mezali 3:5-6).